

za kudumu mu maisha yote! Mungu kwa wazi hazumiliye aina YOYOTE ya bunyanyasaji. Siye, kama kanisa, tunaitwa kutambuwa iyi, KUKUWA mufano ku ulimwengu na kufafana ile

## ¶2706

Numero ya Ombi: 21068-JA-¶2706; Bernadel-Huey, E. Myrna - Oakland, CA, Etats-Unis.

### **Kutunza Kamati ya Mamulaka ya Uchunguzi**

**Adabu ya Mupya ya ¶ 2706.8 – Kutunza Kamati ya Mamulaka ya Uchunguzi**

8. Kutunza Kamati ya Mamulaka ya Uchunguzi. Wakati ya processu ya uchunguzi wakati Muhojiwa ni Askofu, tafauti za mamulaka inaleta seti ya kipekee na ikiwezekana kuwa nguvu ya dynamiques. Kwa ile, baada ya Kamati ya Mamulaka ya Uchunguzi kukamilisha uchunguzi yake na kuwasilisha matokeo yake, banachama kamili na mabadala ambao wameshiriki katika uchunguzi watatolewa, kwa gaarama ya Mamulaka, fursa ya kuelezea buzoefu yabo na mutaalumu mwenye amefunzwa.

#### **Mutazamo:**

Iyi paragraphe ya ziada ya Adabu inaambatana na wito ya mara kwa mara kwa bachungaji kwa ajili ya kujitunza muzuri, hasa baada ya buzoefu yenye mukazo yenye aiko ya kawaida. Kujadiliana ku buzoefu kama ile ni kiwango ya chini yenye inakubalika na bora, kwa sababu ni muhimu kwa processu wa buponyaji kutoka kwabo.

## ¶2715

Numero ya Ombi: 21069-JA-¶2715; Arroyo, Giovanni - Washington, DC, Etats-Unis kwa Commission Mukubwa juu ya Dini na Rangi.

### **Marudiyo ya processu kuhakikisha processu ya aki mu malalamiko kwa dhidi rangi/kabila/tribu ya batu benye biko kiloko**

Ongezeya ¶2715 ya mupya, badilisha namba ya paragraphe inafuata kama inahitajika:

Commission Mukubwa juu ya Dini na Rangi (GCORR) inapashwa kujulishwa wakati malalamiko formal imewasilishwa ku kiwango ya kanisa, na ap dhidi ya mutu wa rangi/ethnique/kabila mudogo mu Mukutano wa Kila Mwaka ndani ya kwenye banaikala. GCORR inapashwa kurudiya tena izi malalamiko. Wakati inahitajika, GCORR inapashwa kuona processu kuhakikisha kwamba processu ya aki inafuatiliwa, na sera za kanisa ya rangi/ethnique/kabila jumuishaji zinafuata. Angaliya, mufano. Kitabu kya Discipline (2026) ¶¶ 4, 5, 140, 162.A. Ile GCORR ao muteuzi wake anapashwa tumika na partis zote wakati ya processu ya malalamiko yote muzima.

#### **Mutazamo:**

Iyi sheriya inahakikisha kwamba processu ya aki na sera ya UMC ya bujumuishaji zinafuata kuhusiana na malalamiko yenye imewasilishwa na processu imefanywa dhidi ya batu ba rangi/ethnique/kabila kidogo. Inaweza wazi piya kwamba GCORR itatumika na partis zote kuhakikisha zimeelewana na sera za kanisa ya processu ya aki na bujumuishaji.